# LEARNING BY EAR

## ”If a tree falls… - Deforestation in Africa"

**EPISODE EIGHT: "FARM is born"**

**AUTHOR: Romie Singh**

**EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz**

**PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis**

**List of characters EPISODE EIGHT:**

**Narrator**

| | |
|---|---|
| **SCENE 1** | **Isi (m, 18)** |
| **SCENE 2** | **Isi (m, 18) Mother (f, 36)** |
| **SCENE 3** | **Talib (m, 20) Chika (f, 18)** |
| **SCENE 4** | **Akiki (f, 7) Chief (m, 36) Sesi (f, 18)** |
| **SCENE 5** | **Chika (f, 18) "Themba" (f, 30) Talib (m, 20) Chief (m, 40) Mulogo (m, 20) Mother (f, 36) Group of Men/Women** |
| **SCENE 6** | **Akiki (f, 7) Isi (m, 18) Sesi (f, 18)** |

## INTRO

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na katika kipindi cha nane cha mchezo wetu mpya kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajipata pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Katika kipindi cha leo, jamii mbili zilizo na mzozo zinatafuta njia za kulima kwa kuzingatia hali ya mazingira na pia kupika kwa kutumia kuni chache. Wakati huo huo Isi anaogopa kwamba huenda hali yake yeye kuzaliwa pacha imesababisha laana katika famila yake.

**Episode EIGHT: "FARM is Born."**

**1.MUSIC UP**

**Scene 1**

**2.ISI NARRATOR:** Wiki hii imekuwa na vituko vyake. Ilianza na taharuki pale Akiki alipokimbia kutoka kambini. Nilikisia kuwa ni kwa sababu ya ndoto aliyoota – kwamba dadake alikuwa amejificha kwenye mti kijiji kwao. Lakini alivyojua mti wa kwenda kutafuta mpaka sasa ni kitendawili. Yeye na Sesi walirudi salama katika kambi ya Dovani. Lakini Sesi angali katika mshtuko. Nimejaribu kumuimbia lakini wapi! Hawezi kuzungumza au tuseme anakataa kuzungumzia-sijui ni vipi. Hajanizungumzia. Ninaogopa asijekuwa na taarifa zisizopendeza.

**3.MUSIC UP**

**Scene 2**

**4. SFX Morning ambience. In the kitchen. Sound of stove, fire crackling**

**5.ISI:** Ma? Unafikiri mambo mabaya hutokea kutokana na walivyofanya mababu zetu? Au wazazi wetu?

**6.MOTHER:** Unazungumzia nini? Hatujafanya jambo lolote baya sisi.

**7.ISI:** Ninafikiria tu Ma, wala usinikasirikie, mimi na Kato ni mapacha. Nyumbani kwetu watu walisema kwamba mapacha wana nguvu za ziada, kwamba tunaweza kuleta bahati au mkosi kulingana na nyota za wazazi wetu. Sijapata kuelewa hayo.

**8.MOTHER:** Mapacha wanapendeza, Isingoma. Wewe na Katu si nuksi. Mmetuletea raha maishani mwetu.

**9.ISI:** Lakini, labda tunaadhibiwa. Pengine ni lazima Kato ateseke kwa kuwa baba yetu alisababisha mzozo miongoni mwa watu wetu. Aliwapatia wauza mbao msitu wetu. Waliiangamiza miti yetu kwa hivyo sisi lazima tulipe.

**10.MOTHER:** Babako alikuwa akijaribu kuwatajirisha watu wetu alipoafikia huo uamuzi. Hakutaka kujitajirisha binafsi. Lakini alihadaiwa na kampuni ya BigWood. Hana uzoefu wa mas-ala ya mikataba na makubaliano.

**11.ISI:** Alikosea tu?

**12.MOTHER:** Naam. Babako ni binadamu. Mababu zetu hawatuadhibu. Tunajiadhibu sisi wenyewe! Kweli Isi. Nakwambia kweli, umasikini na vita ndivyo vinavyotutatiza; si wewe, si Kato wala si babako.

**<u>13.MUSIC UP</u>**

**Scene 3**

**14. SFX: Office sounds / Machine noise of fax**.

**15.TALIB:** Aaah! Hii pepesi (*fax*) imeingia Chika. Kutoka makao makuu ya *Saidia Afrika*.

**16.CHIKA:** Ehe! Inasema nini?

**17.TALIB: (trying to understand the print)** Um…unaweza kuisoma? Macho yako yanaangaza zaidi ya yangu!

**18.CHIKA:** Balaa hii. Si macho yako Talib! Mtambo wetu wa kuchapishia ndo umekwisha wino! Lakini..eem...Acha nitizame. Ukurasa wa mwanzo unaonyesha kwamba ni hati ya mafunzo ya nyanjani.

**19.CHIKA: (Reading slowly)** “Lengo: Kuanzisha usimamizi wa misitu unaoongozwa na jamii.”

**20.TALIB:** Naam, nimekuwa nikisubiri ujumbe huu! Tunahitaji taarifa hizi kuwafunza watu ambao wamekuwa wakipigania haki za malisho pamoja na misitu.

**21.CHIKA:** Kama hao wanaoishi katika kambi hii wanaotoka wilaya za Banega na Abanto!

**22.TALIB:** Ndo hivyo. Usimamizi wa misitu utakaohusisha jamii. Hatua hiyo inahakikisha kwamba kila upande unahusishwa vilivyo, hasa wanawake, watwae umilisi wa rasilimali zao na kutafuta mbinu mwafaka za kuzisimamia,- maanake misitu, mimea na maji. Ni jambo la mashinani. Endelea! Inasema nini?

**23.CHIKA: (Reading slowly and clearly)** “Sehemu ya Kwanza: Jinsi ya kubuni shirika pana la kijamii linalohusisha watu wengi kusimamia misitu; Sehemu ya Pili: Jinsi ya kuwatambua watumizi wote wa misitu na vipi wanavyotumia hiyo misitu.
Sehemu ya Tatu: Jinsi ya kuandaa ramani za misitu, kutathmini rasilimali; Sehemu ya Nne: Jinsi ya kujadiliana mikataba na utekelezaji wa mipango muhimu.”

**<u>24.SFX FAX MACHINE STOPS</u>**

**25.TALIB:** Looo. Kurasa kumi na tano! Kuna mambo mengi sana hapo ya mtu kuelewa, Chika! Lakini kabla hatujawafahamisha wengine, tunahitajika kwanza kusoma.

**26.CHIKA:** Loo! Nina furaha si haba,Talib! Njoo! Tuanze!

**<u>27.MUSIC UP</u>**

## Scene 4

**27a. SFX Daytime ambience inside**

**28.AKIKI:** Sesi? Umeamka?

**29.SESI: (breathes more heavily in response)**

**30.AKIKI:** Chifu Apaloo amekuja kukutembelea kukujulia hali.

**31.SESI: (breathes louder)**

**32.CHIEF APALOO: (gently)**Hujambo mjukuu wangu. Mama Kipko ameniomba nije kwa kuwa mimi nawe ni wa jamii moja. Anadhani huenda hilo litasaidia. Sijaja kufanya lolote jingine! Nataka kuongea nawe tu. Na wewe Akiki pia! Lala kando ya Sesi. Ningependa kuwaambia jambo la kuvutia kuhusu msitu wa Abanto. Ebu fikirieni hiyo miti. Mikubwa na mirefu. Kwa juu matawi na majani yake utadhani ni paa la nyumba. Kila kitu kimewekwa sawa. Katika hali yake ya kiasili.

**33.SESI GIVES A BIG SIGH**

**34.AKIKI: (softly)** Sawa Sesi! Tulia!

**35.CHIEF APALOO:** Huo mti ambao Akiki alikupata ndani,– ungalipo kwa sababu hata mimi kuna wakati nilijificha ndani! Kama ulivyofanya!

**36.SESI (gives an approving grunt)** Hmmm

**37.CHIEF APALOO:** Nilikuwa nikilala kwenye mti kama kawaida yangu wakati wauza mbao walipofika mahali hapo. Nikawasikia wakiulizana ni nani angepanda juu na kuukata mti huo.

**38.AKIKI:** Walikuwa wakitaka kuukata mti huo mkubwa hivyo kwa mikono?

**39.CHIEF:** Naam! Wajinga hao. Tena bila ya idhini. Walikuwa na mnunuzi mjini aliyetaka mti huo akautengezee ngoma. Lakini na mimi pia nilikuwa na ngoma yangu ndogo ambayo niliibeba kila wakati.

**<u>40.SFX AFRICAN DRUMMING</u>**

**41.CHIEF APALOO:** Nilianza kupiga ngoma na kutoa sauti za ajabu ajabu kama vile pepo. Woooooooo….

**42.AKIKI: (laughing)** Hiyo haishtuwi hata kidogo!

**43.CHIEF APALOO:** Inashtua, hasa ukiwa katika msitu wenye giza! Nadhani walifikira kwamba ni pepo aliyekuwa ndani ya mti. Sijapata kuona watu waoga jinsi hiyo. Walitimua mbio za ajabu!

**44.SESI: Happy whimpering sound**

**45.CHIEF APALOO:** Aaha! Sesi! Nakuona unatabasamu! Unaipenda taswira hiyo pia! Kuna hadithi nyingi zaidi kama hiyo. Ninaondoka! Lakini waonaje nikija kukutembelea tena?

**466.AKIKI: (softly)** Kwa hisani yako Chifu, tutembelee tena!

**47.MUSIC UP**

**Scene 5**

**48. SFX Day time ambience outside**

**49.FADE IN MEN AND WOMEN'S VOICES**

**50.CHIKA:** Kwa hivyo hili ni wazo pana. Kama nilivyosema, hili si tena kundi la wanawake tu. Ni shirika la kijamii lililo na wanachama waliochaguliwa kuendesha kamati kadha wa kadha ambazo mtahitajika kubuni. Kusimamia msitu si jambo dogo ati. Naam Themba?

**51.THEMBA:** Unataka tusajili shirika la kijamii na tulifanye kuwa rasmi? Na liwe na jina zuri, sawa?

**52.TALIB:** Wazo zuri hilo! Na? Fikira zozote?

**53.THEMBA: (saying each letter)** F A R M. Maanake Farm kwa maana ya "Forest and Rural Management."

**54.CHIKA:** Themba! Jina zuri hiyo! Kunaye anapinga?

**55.MEN/WOMEN APPROVE:** Nalipenda sana! Wazo zuri! Hongera Themba!

**56.CHIKA:** FARM! Barabara! Tutakapokuwa tayari tutajiandikisha kwa jina FARM na hapo tutaweza kujadiliana kuhusu Mkataba wa Usimamizi wa Misitu. Mkataba huu ni muhimu. Unatufanya sisi kuwa washirika wenza kisheria na makundi mengi yanayomiliki misitu – hata na serikali! Sote tutashiriki kwenye utaratibu wa kidemokrasia wa kuamua jinsi ya kutumia rasilimali za misitu bila kuharibu mazingira.

**57.EXCITED VOICES**

**58.TALIB:** Nadhani kwanza, tuangazie washikadau hao- watu wanaotumia misitu au bidhaa zinazotoka msituni.

**59. VOICES OF APPROVAL**

**60.CHIKA:** Hili ni jedwali lenu mjaze. Katika kisanduku cha upande wa kulia, tafadhalini jazeni majina ya makundi hayo kutegemea ukubwa wayo. Kwa hivyo "Mshikadau wa kwanza” litakuwa kundi kubwa linalotumia msitu kila mara.

**61.CHIEF APALOO:** Tuseme ni wanaoishi wakidunduliza bidhaa za msituni- wanaokwenda kutafuta kuni.

**62.MULOGO:** Wanaotegemea asali kutoka mwituni.

**63.CHIKA:** Na pia waganga wa miti shamba.

**64.TALIB:** Barabara! Jazeni shughuli zao kwenye kisanduku kinachofuata.

**65.MOTHER:** Na kisha, kwenye kisanduku cha kulia tuorodheshe bidhaa tunazopata, siyo?

**66.TALIB:** Naam. Kwa hivyo kwa kipato cha “mshikau wa kwanza ” tuna kuni, asali, dawa na uuzaji wa miti shamba.

**67.CHIEF APALOO:** Na kisha ‘mshikadau wa pili ’ ni kundi kubwa la pili linalofaidika na rasilimali ya misitu.

**68.MOTHER:** Wachungaji, nadhani –walio na mifugo.

**69.MULOGO:** Na ‘mshikadau wa tatu’ pengine ni wapasuaji mbao- wakati miti.

**70.CHIKA:** Sawa. Naam! Tafadhali mshirikiane kwenye makundi na mkubaliane mnachojaza. Tutakutana baada ya nusu saa ili tubadilishane mawazo.

**<u>71.MUSIC UP</u>**

**<u>Scene 6</u>**

**<u>72. SFX Night time ambience outside</u>**

**73.AKIKI:** Mwambie kitendawili hicho, Isi. Ni kizuri sana.

**74.ISI:** Mwambiye wewe mwenyewe Akiki!

**75.AKIKI:** Sawa. Sikiza Sesi! Mti unapoanguka msituni, na hakuna mtu karibu wa kusikia, je mti huo hutoa sauti yoyote?

**76.ISI: (gently)** Unafikiri nini jawabu yake, Sesi?

**<u>77.SESI MAKES A HAPPIER SOUNDING NOISE</u>**

**78.AKIKI: (happy)** Oh Isi, Ameshaaanza! Amerejewa na sauti yake! Atakuwa na uwezo wa kuzungumza hivi karibuni.

**79.ISI: (worried)** Lakini atasema nini pindi akipata sauti!

**<u>80. MUSIC UP</u>**

**OUTRO.**

Ni hayo tuliyokuandalia kwa leo katika kipindi cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* kiitwacho “Mti unapoanguka...”, kilichoandikwa na Romie Singh, kinachoshughulikia suala la uharibifu wa misitu. Jamii zinaunda shirika la usimamizi wa misitu, lakini Isingoma atapata amani?
Usikose kujiunga nasi katika kipindi cha tisa upate kujua mambo yatakavyokuwa.
Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako tafadhali tembelea wavuti www.dw-world.de/lbe

Kwaheri kwa sasa!

**END OF EPISODE 8**